# UJUMBE WA WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO MHE. PROF. MAKAME M. MBARAWA (MB), KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA HALI YA HEWA DUNIANI TAREHE 23 MACHI, 2018

Leo hii Jumuiya ya kimataifa ya hali ya hewa inaadhimisha Siku ya Hali ya Hewa Duniani (World Meteorological Day - WMD). Katika siku hii Dunia inaadhimisha kuanzishwa kwa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (World Meteorological Organization - WMO) tarehe 23 Machi, 1950. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa nchi Mwanachama wa WMO inaungana na wanachama wengine 190 duniani kote kuadhimisha siku hii. Aidha, siku hii inaelezea mchango mkubwa wa taasisi za hali ya hewa kwa ustawi wa jamii, usalama wa maisha na mali kwa kutoa tahadhari za hali ya hewa.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilianzishwa mnamo Desemba, 1999 baada ya Serikali kuchukua uamuzi wa kuboresha utoaji wa huduma muhimu kwa sekta mbalimbali nchini kwa sheria ya Wakala wa Serikali No. 30 ya mwaka 1997. Kabla ya kuanzishwa kwa TMA, huduma za hali ya hewa zilikuwa zikitolewa na iliyokuwa Idara Kuu ya Hali ya Hewa (DoM) iliyoanzishwa kwa Sheria Na. 6 ya mwaka 1978. Kabla ya mwaka 1978, huduma hizo zilikuwa zikitolewa na iliyokuwa Idara ya Hali ya Hewa ya Jumuia ya Afrika Mashariki. Kwa sasa, Serikali iko katika hatua za kuhuisha Sheria ya hali ya hewa na kukamilisha uanzishwaji wa Sera ya Taifa ya Hali ya Hewa kwa utoaji wa huduma bora zaidi za hali ya hewa nchini.

Katika kusherehekea siku ya hali ya hewa kwa Shirika la Hali ya Hewa Duniani, ni desturi kutoa na kaulimbiu ya maadhimisho ya kila mwaka. Hivyo, mwaka huu kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni **'Jiweke tayari na zingatia taarifa za hali ya hewa' (Weather Ready; Climate Smart).** Kaulimbiu hii inaendana na nyakati hizi ambapo jamii kote Duniani inakabiliana na changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi ili kupata suluhisho na kuweka mikakati thabiti ya kukabiliana na changamoto hizo.

**Kujiweka tayari :** Kwa mfano upo mahali ambapo kuna mawingu mazito, mtawanyiko wa radi angani, upepo mkali, mawimbi makubwa baharini au ziwani na mvua kubwa. Je, uko tayari kujihadhari na dhoruba? Je, umefuatilia na kupata tahadhari kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania? Je, unachukua hatua kwa kuzingatia tahadhari hiyo? Je, utaendelea kuwepo mahali ambapo sio salama au utaondoka ili kujiokoa?

Tahadhari ni kipengele muhimu katika kupunguza hatari zitokanazo na hali mbaya ya hewa ambazo ni pamoja na mafuriko, dhoruba, ukame na majanga mengine makubwa. Kabla ya kutokea kwa majanga, tahadhari hutolewa mapema ili jamii iliyopo katika mazingira hatarishi na wale watakaohusika katika kusaidia jamii waweze kujiweka tayari kukabiliana na athari za majanga zinazoweza kujitokeza. Ili mfumo wa utoaji tahadhari ufanye kazi vizuri, inahitajika ushirikishwaji wa watu na jamii iliyopo katika mazingira hatarishi wakiwemo wataalamu wa hali ya hewa, jamii husika, wasambazaji wa tahadhari, vyombo vya habari, waokoaji, wataalamu wa afya, viongozi mbalimbali na watoa maamuzi. Kwa kuhakikisha kuwa kuna uratibu imara wa kupunguza athari za majanga, ushirikishwaji mkubwa wa wadau walio wengi unahitajika. Tanzania kupitia programu ya Kitaifa ya Utoaji Huduma za Hali ya Hewa "National Framework for Climate Services – NFCS" itatoa na mfumo mzuri wa utoaji tahadhari utakao saidia kuwepo na uratibu imara wa kujikinga na maafa miongoni mwa wadau walio wengi nchini ili kulifanya Taifa letu kuwa tayari na kukabiliana na majanga yatokanayo na hali ya hewa.

**Zingatia Taarifa za hali ya hewa :** Kwa mfano upo mahali ambapo kuna ukame unaotokea mara kwa mara. Kama wewe ni Mkulima: Je, utasubiri mvua inyeshe? Au utabadilisha aina ya mazao au utauza mifugo yako kabla ya kufa? Wakulima makini wanaozingatia taarifa za hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania hufanya maamuzi sahihi ya aina ya mbegu za kupanda, wakati mwafaka wa kupanda, kumwagilia, kuvuna, pamoja na maamuzi mengine muhimu katika kilimo. Kama wewe ni mtaalamu wa afya: Je, utakuwa umeandaa vitendea kazi vitakavyosaidia kukabiliana na magojwa yanayosababishwa na hali ya hewa?

Uandaaji wa huduma za hali ya hewa, kuongeza idadi ya wataalamu na wanafunzi wanaojifunza masuala ya hali ya hewa ni hatua mojawapo muhimu ya kujenga jamii inayozingatia matumizi ya taarifa za hali ya hewa. Kwa nchi yoyote, takwimu za hali ya hewa ni muhimu kwa ajili utoaji wa maamuzi katika shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

Mitaala ya mafunzo ya hali ya hewa yatolewayo katika vyuo vyetu nchini imeandaliwa kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na ya baadae katika utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa watoa maamuzi katika sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi ikiwa ni pamoja na Kilimo, Afya, Maji na sekta zingine.

Nia na madhumuni ni kuifanya nchi yetu izingatie matumizi ya taarifa za hali ya hewa katika Nyanja zote za maendeleo. Serikali ya Tanzania itaendelea kuiwezesha Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kuwa na vifaa na mitambo ya kisasa, ya hali ya hewa pamoja na mfumo mzuri wa usambazaji ili huduma za hali ya hewa ziendelee kutolewa kwa wakati kwa manufaa ya maendeleo ya watanzania na nchi yetu kwa ujumla.

Kuongezeka kwa idadi ya watu duniani kunakabiliwa na kuongezeka kwa majanga mbalimbali kama vimbunga baharini, mvua kubwa, joto kali, ukame na mengineyo mengi. Mabadiliko ya hali ya hewa, yanayosababishwa na ongezeko la joto duniani yanasababisha kuongezeka kwa matukio ya hali mbaya ya hewa, kuongezeka kwa kina cha maji ya bahari na ongezeko la hali ya tindikali baharini. Hivyo, kuongezeka kwa idadi ya watu mijini hususan miji iliyopo kwenye mwambao wa bahari kunatuweka kwenye hali ya hatari zaidi. Hivyo, huu ni muda muafaka, tunatakiwa **kujiweka tayari na kuwa makini zaidi kufuatilia taarifa za hali ya hewa wakati wote**.

Nchi yetu kwa kiasi kikubwa mara kwa mara inaathiriwa na majanga mawili makubwa ambayo ni mafuriko na ukame. Mafuriko ni janga la kiasili ambalo mara nyingi husababisha vifo na upotevu wa mali. Kumbukumbu za athari zitokanazo na mafuriko zinaonesha kuwa idadi ya vifo inapungua kwa kiasi na hii ni kutokana pamoja na mambo menginena tahadhari zinazotolewa. Hata hivyo, athari za kiuchumi zimeendelea kuongezeka kutokana na ukosefu wa umakini katika

mipango ya matumizi ya ardhi isiyozingatia matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa.

Ukame ni hali ya ukosefu wa mvua kwa muda mrefu ambayo inaweza kutokea mahali popote duniani. Kwa mujibu wa takwimu za WMO kati ya miaka ya 1970 na 2012 kumekuwa na vifo vya watu takribani 680,000 vilivyotokana na majanga ya ukame yaliyotokea Afrika hususan miaka ya 1975, 1983 na 1984.

Kwa upande wetu, Serikali ya Tanzania inatambua umuhimu wa jukumu lake la kuiwezesha Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ili huduma za hali ya hewa ziendelee kutolewa kwa wakati na kwa munufaa ya watanzania kwa kupunguza athari zinazoambatana na mafuriko na ukame sambamba na nchi **kujiweka tayari na kuzingatia matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa**.

Mwisho, kwa kuzingatia kaulimbiu ya Siku ya Hali ya Hewa Duniani (WMD), napenda kutoa changamoto kwa umma kwamba muwe makini katika matumizi ya huduma za hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania. Aidha, natoa wito kwa wanasayansi, kufanya tafiti katika eneo la hali ya hewa nchini kwa nia ya kuboresha usahihi wa utabiri.

Kwa ujumbe huu ninayofuraha kuwatakia maadhimisho mema yenye mafaniko ya Siku ya Hali ya Hewa Duniani.

**"Jiweke tayari na zingatia taarifa za hali ya hewa"**